# SHA | Social Health Authority

*Bima Bora, Afya Nyumbani*

## Mamlaka ya Afya ya Kijamii

**Mamlaka ya Afya ya Kijamii (SHA)** inaendeleza manufaa yote ambayo NHIF ilikuwa inatoa. NHIF ilishughulikia sehemu ndogo tu ya Wakenya, wengi wao wakiwa wanachama wake wenye mshahara na watu waliojiajiri. SHA inakusudia kupanua manufaa hayo kwa Wakenya **wote** bila kujali viwango vyao vya mapato.

### Umuhimu wa SHA kwa Wakenya ni upi?

SHA, itatoa huduma za kimsingi za afya katika hospitali za Level 2 na 3 chini ya Hazina ya Afya ya Msingi. Kila Mkenya aliyesajiliwa atapata huduma chini ya hazina hiyo ya afya ya msingi, hata kama hajalipa mchango wake.

Kwa wale ambao wamelipa michango yao, kuna manufaa ya ziada yanayojumuisha huduma bora zaidi za wagonjwa wa kutolazwa, wa kulazwa na huduma za dharura, pamoja na bima thabiti kwa ajili ya afya ya akili, magonjwa hatari, upasuaji wa kina na mengine mengi chini ya **SHIF**.

Manufaa mahsusi ya **Linda Mama** na **EduAfya** sasa yameimarishwa! Akina mama wote wajawazito na familia zao watafurahia manufaa hayo chini ya bima iliyoboreshwa. **Edu Afya** pia imepanuliwa kutoka kwa wanafunzi pekee katika shule za sekondari za umma hadi sasa kujumuisha watoto wote wa shule za msingi na sekondari.

---

### Kwanini tunahama kutoka kwa NHIF hadi kwa SHA?

NHIF ilishughulikia tu Wakenya waliokuwa na mishahara, na wengine ambao wangeweza kumudu ada ya bima, hivyo basi kuwezesha wananchi wasiozidi asilimia 20% pekee kuwa na bima ya afya. Kwa sababu hiyo, familia nyingi zinategemea harambee/michango ili kuwezesha mgonjwa wao kutibiwa, hali ambayo husababisha hatari ya kuuza mali za familia ili kulipa bili za matibabu kutoka kwa mifuko yao.

Kwa hivyo, SHA ilibuniwa ili kutoa huduma bora za afya ambazo kila Mkenya anaweza kuzipata. SHA pia imebuni harakati madhubuti ya kidijitali ambayo itaondoa ulaghai na kupigisha Kenya hatua katika azimio la kubuni miundomsingi ya afya ya kiwango cha kimataifa.

SHA itahakikisha kuna usawa kwa Wakenya wote katika ufadhili wa huduma za afya kwani Wakenya watalipa michango sawia na mapato yao. Katika nia ya kutomuacha yeyote nyuma, wale ambao hawawezi kumudu ada ya chini zaidi ya KSh300, watatambuliwa na kulipiwa na serikali.

---

### Kwa nini ujisajili kwenye SHA?

Manufaa ya Mamlaka ya Afya ya Kijamii (SHA) ni hatua nzuri kwa nchi yetu. Pindi unapojisajili hivi, afya ya familia yako inaanza kulindwa. Wagonjwa wa kutolazwa na kulazwa wanashughulikiwa, huduma za ambulensi na huduma za dharura zinatolewa, pamoja na kudhibiti magonjwa hatari hata kama hujakamilisha malipo yako. Kwa nini usubiri zaidi? Jisajili **sasa** kwenye ***147#** au **www.sha.go.ke.**

---

### Ili kunufaika na SHA, gharama yako ni gani?

Mchango wa SHA utakuwa asilimia 2.75 ya mapato ya familia. Kwa mfano, ikiwa mume na mkewe wote wameajiriwa, wote watachangia asilimia 2.75. Kwa wale ambao hawana mshahara, ada nafuu itaamuliwa kulingana na uwezo wao wa kimapato. Kwa familia ambazo haziwezi kumudu ada ya chini ya KSh300, Serikali itazilipia.

Mamlaka ya Afya ya Kijamii itatekeleza majukumu yake kupitia Hazina 3:

- Hazina ya Huduma za Afya ya Msingi (PHC)
- Hazina ya Bima ya Afya ya Kijamii (SHIF)
- Hazina ya Hali za Dharura, Magonjwa Sugu na Hatari (ECCIF)

## Manufaa ya Hazina ya SHA (PHC)

Katiba yetu inamhakikishia kila Mkenya huduma ya kimsingi ya afya. Hii itafaulishwa kupitia Hazina ya Afya ya Msingi ya SHA, ambayo nayo itahakikisha huduma kwa wote bila kujali hali yake ya ulipaji ada. Huduma zilizo chini ya Hazina hii zinapatikana BILA MALIPO katika vituo vya afya vya Level 2 na 3 kwa watu waliosajiliwa, isipokuwa kwa hali changamano, masharti magumu yatamhitaji mhusika kuwa amelipa ada. Manufaa yake yanajumuisha:

| | |
|---|---|
| **Wasiokuwa wa kulazwa** | Ushauri, vipimo vya maabara, dawa, ushauri na usaidizi wa kiakili, chanjo za KEPI, na huduma kwa wajawazito ikiwemo kujifungua. |
| **Vipimo vya maabara** | Vipimo vya hali za kawaida na vipimo mahsusi kama vile kuchunguza saratani. |
| **Macho** | Vipimo vya macho na matibabu yake, na kutolewa kwa miwani ya macho kwa watoto walio na umri usiozidi miaka 18. |
| **Mochari (Mortuary)** | Huduma za mochari na uhifadhi wa mwili. |
| **Kulazwa** | Matibabu ya kulazwa katika hospitali ya **Level 3.** Haya yatajumuisha gharama za kulazwa, eksirei (X-ray) na uchunguzi wa ndani ya mwili (ultrasound), dawa, unyooshaji wa viungo, oksijeni, damu, na ufuatiliaji baada ya kuruhusiwa kuondoka. |

## Manufaa ya SHA (ECCIF)

Huduma za dharura kwa Wakenya wote zitatolewa. Ili kuhakikisha kuwa familia hazifilisishwi na ugonjwa kama vile saratani, ugonjwa wa figo unaohitaji kusafishwa damu, na hali nyinginezo kama hizo, SHA pia itasimamia ECCIF.

Faida za ECCIF zinajumuisha:

| | |
|---|---|
| **Ambulensi** | Usafiri hadi hospitali iliyo karibu. |
| **Dharura** | Bima hii itasimamia mshtuko wa moyo, shida ya kupumua, kiwewe kikubwa, mshtuko, kifafa, kuumwa na nyoka, au kuumwa na mbwa. |
| **Magonjwa hatari** | Kulazwa katika kitengo cha magonjwa hatari, kwenye sadaruki (ICU na HDU), katika hospitali za **Level 4 hadi Level 6.** |
| **Ufifishaji maumivu** | Kuimarisha ubora wa maisha ya wagonjwa walio na magonjwa sugu au ya kutishia maisha. |
| **Vifaa vya wenye mapungufu** | Utoaji wa vifaa vya kusikia kwa watoto wasiozidi umri wa miaka 18, viti vya magurudumu, mikongojo, viatu vya miguu iliyopinda, fremu za kutembea, na viatu vya tiba. |
| **Magonjwa sugu** | Huduma hii inashughulikia kulazwa, tiba ya figo (dialysis), tiba baada ya kupandikizwa figo, udhibiti wa saratani, usaidizi wa afya ya akili kwa wagonjwa. |

## Manufaa ya Hazina ya Bima ya Afya ya Kijamii (SHIF)

Hazina ya Bima ya Afya ya Jamii itatekeleza majukumu sawa na yale ya NHIF, kwa kuunganisha rasilimali ili kufidia Wakenya wote chini ya Kifurushi cha Manufaa Muhimu cha SHA, kulingana na malengo ya Mpango wa Afya kwa Wote (UHC). Faida za SHIF zinajumuisha:

| | |
|---|---|
| **Wasiokuwa wa kulazwa** | Huduma zilizoimarishwa za wagonjwa wasiokuwa wa kulazwa, zinazojumuisha uchunguzi wa maabara kwa ugonjwa wa kisukari, ugonjwa wa moyo, anemia ya selimundu, na pumu katika hospitali za **Level 4 hadi 6,** zitatolewa. |
| **Wagonjwa wa kulazwa** | Udhibiti wa ugonjwa unapokuwa umelazwa katika hospitali za **Level 4 hadi 6.** Hii itajumuisha gharama za kulazwa, x-ray na ultrasound, dawa, unyooshaji viungo, oksijeni, damu, na ufuatiliaji baada ya kuachiliwa hospitalini. |
| **Kinamama Wajawazito (Maternal)** | Inahusu hospitali za **Level 2 hadi 6** kwa kujifungua kwa kawaida na kupasuliwa, wa usaidizi na wa mwisho; huduma ya baada ya kujifungua kwa mama na mtoto mchanga; gharama za upasuaji, matibabu na wodi ya kujifungua; vipimo vya maabara, bidhaa za damu na oksijeni; kudhibiti maambukizi, mshtuko/madhara ya kujifungua, hali zinazohusiana na kujifungua na upangaji uzazi. |
| **Figo** | Inashughulikia matibabu yaliyoimarishwa, katika hosptali za Level **3 hadi 6,** kuhusu magonjwa yanayohusiana na figo, vipimo vya maabara vya kawaida, uingizaji na utoaji wa kifaa cha kutoa mkojo (catheter), dawa, ushauri na ukaguzi, upandikizaji wa figo unaojumuisha huduma za kabla na baada ya upasuaji. |
| **Upigaji picha za kimatibabu** | Inashughulikia upigaji picha za MRI, CT Scans, Mammografia, Echo, EEGs, uchunguzi maalum wa ndani ya mwili (ultrasound), kukagua na kuripoti matokeo ya picha. |
| **Upasuaji** | Hushughulikia huduma katika hospitali za Level **3 hadi 6** kwa wagonjwa wa kulazwa na huduma za kabla ya upasuaji; viwango vyote vya upasuaji vikijumuisha taratibu maalum kama vile vipandikizi vya viungo na vipandikizi bandia; huduma zinazohitajika zinazohusiana na utaratibu husika; vipimo vinavyohitajika, na huduma za baada ya upasuaji. |
| **Tiba ya kansa/ saratani** | Hushughulikia huduma katika hospitali za **Level 3 hadi 6** kwa matibabu ya radiotherapy, chemotherapy na matibabu mengine, vifaa vya matumizi ya tiba, uchunguzi wa maabara, bidhaa za damu, taratibu za upasuaji, na zaidi. |
| **Matibabu ya ng'ambo** | Inashughulikia taratibu za matibabu na upasuaji ambazo hazipatikani nchini Kenya. |

Dawa za ARVs, za malaria, TB, na vipimo andamani, pamoja na huduma za upangaji uzazi, na chanjo za KEPI zitakuwa zinatolewa katika hospitali ambazo zimeunganishwa na mfumo wa HIE.

**Kwa maelezo zaidi, tafadhali tembelea Ofisi za SHA zilizo karibu nawe au piga simu 0800 720 601**

**Ili Kujiandikisha**

**Finya *147#**

**Au tembelea**

**www.sha.go.ke**